

*Amri ya Mamlaka ya Maji Safi Na Usafi wa Mazingira Lindi ("Lindi WSSA")  
la Bei Za Mpito Za Huduma Za Usafi wa Mazingira*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 63 la tarehe 28/1/2022

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA  
(SURA NA 272)

**AMRI**

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 29(1)(d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA LINDI ("LINDI WSSA") LA BEI ZA MPITO ZA HUDUMA ZA USAFI WA MAZINGIRA, 2022

- Jina 1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi ("Lindi WSSA") ya Bei za Huduma za Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2022.
- Marekebisho ya Bei 2. Bei za huduma za usafi wa mazingira za Lindi WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali ya Amri hii.
- Masharti 3. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:
- (a) ifikapo tarehe 30 Juni 2022 au kabla, Lindi WSSA itawasilisha kwa EWURA ombi la marekebisho ya bei kwa miaka mitatu ikiwa ni pamoja na bei za huduma za usafi wa mazingira kulingana na gharama zitakazoainishwa kwenye mpango wa bishara wa mamlaka; na
- (b) Lindi WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Lindi WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Lindi WSSA katika siku zijazo.

*Amri ya Mamlaka ya Maji Safi Na Usafi wa Mazingira Lindi (“Lindi WSSA”)  
la Bei Za Mpito Za Huduma Za Usafi wa Mazingira*

*Tangazo la Serikali Na. 63 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

JEDWALI LA KWANZA: TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei Zilizoidhinishwa za Uondoaji wa Majitaka

| Kundi la Wateja | Tozo Zilizoidhinishwa<br>2021/22 |  |
|-----------------|----------------------------------|--|
|                 | Shilingi kwa Mita ya Ujazo       | Shilingi kwa Tripu (Gari la unit<br>5) |
| Majumbani       | 30,000                           | 150,000                                |
| Taasisi         | 30,000                           | 150,000                                |
| Biashara        | 30,000                           | 150,000                                |
| Viwanda         | 32,000                           | 160,000                                |

Jedwali Namba 1.2: Bei Zilizoidhinishwa za Kumwaga Majitaka Kwenye Mabwawa ya Lindi WSSA

| Kundi la Wateja | Tozo Iliyoidhinishwa (Shilingi kwa Gari)<br>2021/22 |
|-----------------|---|
|                 | Magari Yote   |

Dodoma,  
19 Januari, 2022

GODFREY H. CHIBULUNJE  
*Mkurugenzi Mkuu*